**KAULI YA TAARIFA YA CHANJO**

# Chanjo ya Kichaa cha mbwa:

***Unachohitaji Kujua***

Many Vaccine Information Statements are available in Swahili and other languages. See www.immunize.org/vis

Kauli nyingi za taarifa ya chanjo zinapatikana katika Kiswahili na lugha nyinginezo. Angalia www.immunize.org/vis

## 1. Kwanini unahitaji kuchanjwa?

**Chanjo ya kichaa cha mbwa** inaweza kuzuia **kichaa cha mbwa**.

Kichaa cha mbwa ni ugonjwa hatari ambao karibu wakati wote husababisha kifo.

Virusi vya kichaa cha mbwa huambukiza mfumo mkuu wa neva. Dalili zinaweza kujitokeza kuanzia masiku hadi miaka baada ya mfiduo kwa virusi hivyo na zinajumuisha kichaa (kuchanganyikiwa), tabia isiyo ya kawaida, maruerue, haidrofobia (kuogopa maji), na insomnia (kukosa usingizi), ambavyo hutangulia kuwa mahututi na kifo.

Watu wanaweza kupata kichaa cha mbwa ikiwa watagusana na mate au tishu za neva za mnyama aliyeambukizwa, kwa mfano kupitia kwa kuumwa au kukwaruzwa, na ukose kupata uuguzi wa matibabu unaofaa, ikijumuisha chanjo ya kichaa cha mbwa.

## 2. Chanjo ya kichaa cha mbwa

Baadhi ya **watu walio katika hatari kubwa ya mfiduo kwa kichaa cha mbwa, kama vile wale wanaofanya kazi na wanyama wanaoweza kuwa wameambukizwa, wanapendekezewa kupokea chanjo** ili kusaidia kuzuia kichaa cha mbwa iwapo mfiduo utatokea. Ikiwa uko katika hatari kubwa ya mfiduo kwa virusi vya kichaa cha mbwa:

- Unapaswa kupokea dozi 2 za chanjo ya kichaa cha mbwa inayopeanwa katika siku za 0 na 7.
- Kwa kutegemea na kiwango chako cha hatari, huenda ukashauriwa kufanyiwa kipimo kimoja au zaidi cha damu au upokee dozi ya nyongeza ndani ya miaka 3 baada ya dozi 2 za kwanza. Mtoa huduma za afya wako anaweza kukupatia maelezo zaidi.

**Chanjo ya kichaa cha mbwa inaweza kuzuia kichaa cha mbwa ikiwa itapeanwa kwa mtu baada ya mfiduo**. Baada ya mfiduo au mfiduo unaowezekana kwa kichaa cha mbwa, eneo la kidonda linapaswa kusafishwa kabisa kwa sabuni na maji. Ikiwa mtoa huduma za afya wako au idara ya afya ya eneo watapendekeza kuchanja, hiyo chanjo inapaswa kupeanwa haraka iwezekanavyo baada ya mfiduo lakini inaweza kufanya kazi wakati wowote kabla ya dalili kuanza. Mara tu dalili zinapoanza, chanjo ya kichaa cha mbwa haisaidii tena katika kuzuia kichaa cha mbwa.

- Ikiwa haujachanjwa dhidi ya kichaa cha mbwa hapo awali, unahitaji dozi 4 za chanjo ya kichaa cha mbwa ndani ya wiki 2 (zikipeanwa siku za 0, 3, 7, na 14). Pia unapaswa kupata dawa nyingine inayoitwa immunoglobulin ya kichaa cha mbwa katika siku ile unapokea dozi ya kwanza ya chanjo ya kichaa cha mbwa au punde baadaye.
- Ikiwa umepokea chanjo ya kichaa cha mbwa hapo awali, kwa kawaida unahitaji tu dozi 2 za chanjo ya kichaa cha mbwa baada ya mfiduo.

Chanjo ya kichaa cha mbwa inaweza kupeanwa wakati mmoja na chanjo zingine.

## 3. Zungumza na mtoa huduma za afya wako

Mwambie mtoa huduma ya chanjo wako ikiwa mtu anayepokea chanjo:

- Amekuwa na **mmenyuko wa mzio baada ya dozi ya awali ya chanjo ya kichaa cha mbwa**, au ako na **mmenyuko wowote mbaya sana wa mzio, wa kutishia maisha**
- Ako na **mfumo dhaifu wa kinga**
- Anatumia **au anapanga kutumia chloroquine au dawa inayohusiana na chloroquine**
- Amepokea **chanjo ya kichaa cha mbwa hapo awali** (mtoa huduma wako atahitaji kujua ni lini ulipokea dozi zozote za chanjo ya kichaa cha mbwa hapo awali)

U.S. Department of Health and Human Services
Centers for Disease Control and Prevention

Katika baadhi ya visa, mtoa huduma za afya wako anaweza kuamua kuahirisha chanjo ya kawaida ya kichaa cha mbwa (kabla ya mfiduo) hadi katika ziara ya baadaye. Au mtoa huduma za afya wako huenda akafanya kipimo cha damu kabla au baada ya chanjo za kichaa cha mbwa kupeanwa ili kutathmini kiwango chako cha kinga dhidi ya kichaa cha mbwa.

Watu walio na magonjwa madogo madogo, kama vile mafua, wanaweza kuchanjwa. Watu ambao ni wagonjwa kwa wastani au wagonjwa vibaya wanapaswa kwa kawaida kungojea hadi wapone kabla ya kupokea dozi ya kawaida (kabla ya mfiduo) ya chanjo ya kichaa cha mbwa. **Ikiwa umekuwa na mfiduo kwa virusi vya kichaa cha mbwa, unapaswa kuchanjwa pasipo kujali ugonjwa wako wa sasa, ujauzito, unyonyeshaji, au mfumo dhaifu wa kinga.**

Mtoa huduma za afya wako anaweza kukupatia habari zaidi.

## 4. Hatari za mzio dhidi ya chanjo

- Maumivu, wekundu, kufura, au mjikuno kwenye eneo lililochomwa sindano, na maumivu ya kichwa, kichefuchefu, maumivu ya tumbo, maumivu ya misuli, au kizunguzungu vyaweza kutokea baada ya chanjo ya kichaa cha mbwa.
- Mabaka, maumivu katika maungo, au joto jingi wakati mwingine hutokea baada ya dozi za nyongeza.

Watu huzirai wakati mwingine baada ya taratibu ya kimatibabu, ikijumuisha uchanjwaji. Mwambie mtoa huduma wako ikiwa unahisi kisunzi au mabadiliko katika kuona kwako au kuhisi milio masikioni.

Kama ilivyo na dawa yoyote ile, kuna uwezekano nadra sana kwa chanjo kusababisha mmenyuko mbaya wa mzio, majeraha mengine mabaya, au kifo.

## 5. Na je, kukiwa na tatizo hatari?

Mmenyuko wa mzio unaweza kutokea baada ya mtu aliyechanjwa kuondoka kliniki. Ikiwa utaona ishara za mmenyuko mbaya wa mzio (mabaka, kuvimba uso na koo, matatizo ya kupumua, moyo kudunda kwa kasi, kizunguzungu, au udhaifu), pigia simu **9-1-1** ili mtu huyo apelekwe kwenye hospitali iliyo karibu.

Kuhusu ishara zingine ambazo zinakupatia wasiwasi, pigia simu mtoa huduma za afya wako.

Mizio hatari inapaswa kuripotiwa kwa Mfumo wa Kuripoti Matukio Mabaya ya Chanjo (Vaccine Adverse Event Reporting System - VAERS). Mtoa huduma za afya wako kwa kawaida ataweka faili ya ripoti hii, au unaweza kufanya hivyo mwenyewe. Tembelea tovuti ya VAERS katika **www.vaers.hhs.gov** au piga simu **1-800-822-7967**. *VAERS ni ya kuripoti mizio pekee, na wafanyikazi wa VAERS hawapeani ushauri wa kimatibabu.*

## 6. Je, ninawezaje kujifunza mengi zaidi?

- Muulize mtoa huduma za afya wako.
- Pigia simu idara ya afya eneo lako au ya jimbo.
- Tembelea tovuti ya Utoaji wa Chakula na Dawa (Food and Drug Administration - FDA) upate machapisho ya vifurishi vya chanjo na taarifa ya ziada katika **www.fda.gov/vaccines-blood-biologics/vaccines**.
- Wasiliana na Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa (Centers for Disease Control and Prevention - CDC:
  - Pigia simu **1-800-232-4636 (1-800-CDC-INFO)** au
  - Tembelea tovuti ya CDC ya kichaa cha mbwa katika **www.cdc.gov/rabies**

Swahili translation provided by Immunize.org